

HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO



TENDER BOARD CIRCULAR RESOLUTION.

14/01/2022

KUTOKA: KITENGO CHA MANUNUZI.

KWENDA: WAJUMBE WA BODI YA ZABUNI.

YAH: ZABUNI YA KAZI ZA UJENZI JENGO LA EMD NA NYUMBA YA MTUMISHI 3 IN ONE HOSPITALI YA WILAYA

Kanuni ya Manunuzi namba 446 za mwaka 2013 ibara ya 58 ibara ndogo ya 1&2 inaelekeza bodi ya zabuni kufanya maamuzi bila ya kuitisha kikao inapitisha kwa njia ya kuzungusha jalada.

Kitengo cha Manunuzi kilifungua zabuni mbili kuitia njia ya mfumo wa manunuzi mtandaoni (Tanneps) mnamo tarehe 11/01/2022, Zabuni namba **LGA/044/2021/2022/W/10** ya ujenzi wa Jengo la Emmergency Medical Department na Zabuni namba LGA/044.2021/2022/W/11 ya ujenzi wa Staff house 3 in one katika Hospiatali ya Wilaya Kijiji cha Kiwanda kata ya Kirongo Samanga,Kazi hizo zimeletwa na maelekezo ya wizara yanayoelekeza kuwa zabuni itangazwe kwa kutumia Zabuni ya ushindanishi ya Kitaifa (National Competitive Tendering) ambapo kwa zabuni ya ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa dharura (Emergency Medical Department) wazabuni wakandarasi wenye sifa ya kusajiliwa na Bodi ya wakandarasi kuanzia daraja la nne na kuendelea ndio wanaruhusiwa kushiriki zabuni hio inayotarajiwa kutangazwa, zabuni ya ujenzi wa Jengo la nyumba ya watumishi (Staff house 3 in one) wazabuni wakandarasi wenye sifa ya kusajiliwa na Bodi ya wakandarasi kuanzia daraja la sita na kuendelea ndio wanaruhusiwa kushiriki zabuni.

Katika Ufunguzi huo wazabuni sita walishiriki kila Zabuni kama ifuatavyo:

Zabuni namba LGA/044/2021/2022/W/10 ya ujenzi wa Jengo la Emmergency medical department, wazabuni walioshiriki ni:

- SARO BUILDERS LTD - **608,443,665.50**
- MALAMLA ENTERPRISES CO.LTD- **1,519,996,072/=**
- GEMINI ENGINEERING AND CONSTRUCTION **1,143,559,594/=**
- KADIVA-12 GROUP LTD **661,973,392/=**
- RAVJI CONSTRUCTION LTD **1,458,861,352/=**
- KWIZOMBE BUILDERS LTD **698,901,250/=**

Baada ya ufunguzi zabuni hii ilifanyiwa tathmini (evaluation) kwa njia ya mfumo wa Tanneps ambapo kamati ya tathmini ilijiridhisha kuwa wazabuni walioshiriki walikua na ofa ya juu ya makisio ya mhandisi kwa Zaidi ya asilimia 100%, Mzabuni alietenda bei ya chini alikua na Tsh. 608,561,665.50 wakati makisio ya Mhandisi kwa kazi ya ujenzi wa jengo la EMD yalikua Tsh.

300,000,000/=. Kitengo cha Manunuzi kinapendekeza Zabuni hii itangazwe upya au zitumike njia mbadala za ununuzi kama Single source Procurement na Force account kwa kuzingatia uharaka wa utekelezaji wa Ujenzi huo.

Zabuni namba LGA/044.2021/2022/W/11 ya ujenzi wa Staff house 3 in one

- RAVJI CONSTRUCTION LTD **571,391,990/=**
- SARO BUILDERS LTD **232,755,896.80**
- TRUSTBUILD CONSTRUCTION CO. LTD **241,855,600/=**
- GEMINI ENGINEERING AND CONSTR. LTD **714,831,020/=**
- MALAMLA ENTERPRISES CO. LTD **489,073,809.40/=**
- 3D BUILDERS LTD **334,827,060/=**

Baada ya ufunguzi zabuni hii ilifanyiwa tathmini (evaluation) kwa njia ya mfumo wa Tanneps ambapo kamati ya tathmini ilijiridhisha kuwa wazabuni walioshiriki walikua na ofa ya juu ya makisio ya mhandisi kwa Zaidi ya asilimia 80%, Mzabuni alietenda bei ya chini alikua na Tsh. 167,413,530.00 wakati makisio ya Mhandisi kwa kazi ya ujenzi wa jengo la Nyumba ya Mtumishi 3 in one yalikua Tsh. 90,000,000/=. Kitengo cha Manunuzi kinapendekeza Zabuni hii itangazwe upya au zitumike njia mbadala za ununuzi kama Single source Procurement na Force account kwa kuzingatia uharaka wa utekelezaji wa Ujenzi huo

Nawasilisha kwenu Wajumbe wa Bodi ya Zabuni ili muweze kupitia na kuitisha mapendekezo haya ili kuendelea na taratibu nyingine.

Taarifa za tathmini za zabuni tajwa hapo juu zimeambatanishwa.

Na	JINA LA MJUMBE WA BODI YA ZABUNI	UAMUZI WA KILA MJUMBE		MAPENDEKEZO YA MJUMBE WA BODI YA ZABUNI	SAHIHI
		NDIO	HAPANA		
1.	Patricia P.Kinyange	✓		Taratibu zendelee	PL
2.	Judith P. Mahende	✓		Taratibu zendelee	Q
3	Emmanuel S. Martin	✓		Taratibu re Mamnuu zendelee	F
4	Chrispin Mng'anya				
5	Thomas B. Zakayo	✓		Taratibus zendelee Kura Taratibus zote	EB


RASHID KIMWERI

Katibu wa Bodi ya Zabuni

H/W ROMBO